MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Uchanganuzi wa Sauti za Vijana katika Tamthilia ya Kiswahili; Mfano katika Tamthilia za Mstahiki Meya na Bembea ya Maisha

Riro Matinde Samwel[1] Kasuma Roseline[2]
[1]Chuo Kikuu cha Kisii, riromatinde2020@gmail.com
[2]Chuo Kikuu cha Rongo, rosekasuma@yahoo.com

**IKISIRI**

Tamthilia kama mojawapo ya tanzu za fasihi andishi ni kioo cha jamii. Hii ni kwa misingi kwamba tamthilia huelimisha jamii kuhusu mila na tamaduni zinazoelekeza mahusiano ya wanajamii, maendeleo, mazingira, uongozi na mengineyo. Elimu ipatikanayo kupitia fasihi husawiri muono ulimwengu wa jamii husika. Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa pamoja na kuwa maendeleo ya vijana katika jamii yanawiana na uhusika wao katika kuikuza jamii, ni tafiti chache ambazo zimelenga nafasi na uhusika wa vijana katika fasihi ya Kiswahili. Ni kutokana na ukweli huu ambapo makala hii inachanganua sauti za vijana wa kike na wa kiume kuhusu mabadiliko ya kijamii katika tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Bembea ya Maisha* (Arege, 2022) za Timothy Arege. Makala hii inajikita kwenye: dhamira, maudhui, lugha na wahusika (uhusika) vijana wa kike na wa kiume. Kazi hii itaongozwa na mihimili ya nadharia ya uhalisia. Tamthilia hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa kuzingatia kuwa mwandishi ni wa karne ya 21. Kazi hizi zimeangazia masuala yanayowakumba vijana kwenye karne 21. Aidha, tamthilia hizi zimekuwa zikitahiniwa katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne (KCSE) nchini Kenya pamoja na kuigizwa katika majukwaa mbalimbali. Hili limefanya tamthilia hizi kuwa chachu na kuwapevua mawazo yao kuhusu jamii wanamoishi. Utafiti huu ulikuwa wa kiuthamano. Njia ya ukusanyaji wa data ilikuwa ni kuhakiki matini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Malengo ya makala hii ni kubainisha sauti ya vijana kuhusu mabadiliko ya kijamii katika kazi zilizoteuliwa. Kazi hii itakuwa mchango katika ulingo wa fasihi, elimu, wasomi wanaoshughulikia masuala ibuka katika jamii na jamii kwa jumla.

**KUHUSU MAKALA**

***Maneno Muhimu:***
Mabadiliko, Sauti ya Vijana, Tamthilia, Vijana

***Historia ya Makala:***
*Tarehe ya Kutumwa: 24 Jan 26*
*Tarehe ya Kurekebishwa: 07 Aprili 2026*
*Tarehe ya Kukubalika: 03 Juali 2026*
*Mtandaoni: 29 Agosti 2026*

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254721571748; *Barua Pepe* riromatinde2020@gmail.com
Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Riro, M.S.& Kasuma, R. (2026). Uchanganuzi wa Sauti za Vijana katika Tamthilia ya Kiswahili; Mfano katika Tamthilia za Mstahiki Meya na Bembea ya Maisha. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(2), 59-69
© 2026
Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA)

## 1. Utangulizi

Vijana, wakiwa sehemu muhimu ya jamii, mara nyingi hukumbana na changamoto si haba kama vile; ukosefu wa ajira, rushwa, na kutengwa kisiasa. Mathalan, changamoto hizi zilipelekea vijana almaarufu Gen Z nchini Kenya kuwa sauti yenye nguvu kwa kusukuma mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi kupitia maandamano, mitandao ya kijamii, na hata kuanzisha vyama vipya vya kisiasa kama vile *47 Voices of Kenya Congress* mnamo mwaka wa 2025. Tamthilia, kama kioo cha jamii, huakisi hali hizi, ingawa uhalisi wa uwakilishi wao unahitaji uchunguzi wa kina (Wamitila, 2003). Makala hii inachunguza namna sauti ya vijana inavyojitokeza katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea tamthilia za: *Mstahiki Meya* (Arege, 2009) na *Bembea ya Maisha* (Arege, 2022) zilizotungwa na Timothy Arege. Lengo kuu ni kubaini jinsi mwandishi huyu anavyotumia wahusika vijana kutoa maoni yao kuhusu masuala ya kijamii, elimu, siasa na uchumi. Waaidha, makala inadhirisha namna sauti ya vijana inavyowakilishwa katika fasihi ya Kiswahili, kwa kujikita katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha*. Kazi hizi zinatoa fursa ya kuchunguza masuala yanayowakabili vijana, matarajio yao, na jinsi wanavyoshughulikia mazingira yao ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Uchambuzi unaonyesha kuwa fasihi ni jukwaa muhimu la kuwasilisha hisia na fikra za vijana, na kwamba tamthilia hizi mbili zinatoa mchango wa kipekee katika kuelewa nafasi ya vijana katika muktadha wa kijamii na kisiasa (Njoroge, 2023; Mwangi, 2021).

Tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha* ni mifano bora inayodhihirisha namna vijana wanavyojitokeza kama wahusika wenye msimamo, fikra pevu, na ari ya kupigania mabadiliko ndani ya jamii. Katika fasihi ya Kiswahili, sauti ya vijana inachukua nafasi muhimu katika kuonyesha mitazamo, hisia, na changamoto wanazokabiliana nazo katika jamii. Katika kazi za kifasihi kama vile *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha* sauti hii inaonekana dhahiri shahiri kupitia wahusika na maudhui yanayozungumziwa na mtunzi.

## 2.0 Fasihi ya Kiswahili

Wataalam wa Kiswahili wamefafanua dhana ya Fasihi kwa kuzingatia misingi mikuu miwili: Umbo na uamilifu/ujumbe. Wataalamu wengi huangazia matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa njia ya kipekee na ya ufundi. Wamitila (2003) anafafanua fasihi kama sanaa ya lugha. Anasisitiza kwamba fasihi hutumia lugha kwa njia ya ubunifu na ya kisarufi ili kuwasilisha tajriba ya maisha ya binadamu. Hivyo, Fasihi ya Kiswahili inatambulika kupitia matumizi ya Kiswahili sanifu au lahaja zake katika uwasilishaji huo wa kisanaa. Balisidya (1987) anaieleza fasihi kama uumbaji unaojumuisha kazi zenye ubunifu wa hali ya juu na utumiaji wa lugha kwa ustadi unaovutia. Katika muktadha wa Kiswahili, huu ni ufundi wa kutunga hadithi, mashairi, au tamthilia kwa lugha hiyo.

Kwa upande mwingine, kuna wataalam ambao hukita fasiri yao kwa kuzingatia jukumu la kijamii la fasihi. Mohamed na Mazrui (1992) wanaeleza fasihi kwa kuzingatia uhusiano wake na jamii. Wanatazama fasihi kama kioo cha jamii, ikionyesha na kuakisi utamaduni, historia, na hali halisi ya maisha ya jamii ya Waswahili na wazungumzaji wa lugha hiyo. Mbuguni (1996) anasisitiza kwamba fasihi huwasilisha ujumbe wa msanii kwa jamii. Ujumbe huu unaweza kuwa elimu, uhifadhi wa utamaduni, au uhamasishaji wa mabadiliko. Kwa hivyo, Fasihi ya Kiswahili hutumika kama njia ya mawasiliano na hifadhi ya maarifa ya jamii.

## 3.0 Fasihi na Jamii

Uhusiano kati ya fasihi na jamii ni wa karibu, wa kiini, na wa kutegemeana; fasihi huonekana kama kioo cha jamii, huku jamii ikiwa chanzo kikuu cha maudhui ya fasihi. Kwa kurejelea wataalam mbalimbali, uhusiano huu unaweza kufafanuliwa kupitia majukumu makuu mawili: fasihi huakisi jamii na fasihi huathiri/huunda jamii. Wataalam wengi huona fasihi kama kiwakilishi cha ukweli na hali halisi za jamii, ikifuata nadharia ya uhalisia. Kwa mfano, Mohamed na Mazrui (1992) wanasisitiza kwamba fasihi ni kioo cha utamaduni, historia, na falsafa ya jamii husika.

Mwandishi huchagua matukio, wahusika, na mazingira kutoka katika jamii na kuyabadilisha kuwa kazi ya sanaa. Kwa mfano, riwaya, tamthilia na ushairi wa Kiswahili huakisi changamoto za rushwa, ukosefu wa ajira, au migogoro ya kisiasa inayowakabili Waafrika. Wamitila (2003) anaeleza kuwa fasihi huchota tajriba ya maisha ya binadamu na kuyawasilisha tena kwa lugha ya kisanaa. Kazi za fasihi husaidia kuhifadhi na kueleza mila, desturi, na mwingiliano wa kijamii unaoikumba jamii. Eagleton (2008), katika uhakiki wake wa

kijamii anabainisha kuwa fasihi huakisi miundo ya kiuchumi na kisiasa ya wakati fulani. Kwa hiyo, fasihi huweza kufichua uonevu na matabaka ya kijamii yaliyofichika.

Kwa upande mwingine, zaidi ya kuakisi, fasihi ina uwezo wa kushawishi, kuelimisha, na kuhamasisha mabadiliko, hivyo kuwa kikolezo cha maendeleo. Ngũgĩ (1986) katika kazi zake, anasisitiza jukumu la fasihi katika kuhamasisha na kuunda uharakati wa kisiasa na kutetea utamaduni dhidi ya ukoloni au ukandamizaji. Kwake, fasihi inapaswa kuwa silaha ya mapambano. Mbuguni (1996) anabainisha kuwa fasihi huwasilisha ujumbe wa msanii kwa jamii kwa lengo la kuelimisha na kuonya. Inatumika kama njia ya ufunzaji na kurekebisha tabia, huku ikiunda maadili mapya katika jamii. Lukács (1971) katika muktadha wa uhalisia, anasisitiza kwamba fasihi bora inapaswa si tu kuakisi bali pia, kuonyesha uwezekano wa mabadiliko katika jamii. Fasihi humwandaa msomaji kufikiri kwa kina na kutamani ulimwengu bora.

Kutokana na mitazamo hii miwili, uhusiano kati ya Fasihi na Jamii ni wa kimuktadha na kimajukumu. Jamii hutoa malighafi (maudhui) kwa fasihi, huku fasihi ikiirejeshea jamii picha iliyochambuliwa na iliyopambwa kisanaa (ujumbe) ili kuisaidia kuelewa, kurekebisha, na kujenga maisha yake. Vijana kama wahusika katika kazi ya fasihi huwa ni wawakilishi wa jamii inayosawiriwa na mwandishi. Hivyo basi, sauti yao katika fasihi huwa na uamilifu wa kujenga na kuendeleza uhalisia wa kijamii

## 4.0 Misingi ya Nadharia

Uhalisia ni nadharia inayotoa picha au taswira halisi ya maisha ya kawaida ya binadamu katika jamii. Maisha hayo yanachukuliwa kuwa ya kawaida na yenye ukweli, yaliyotendeka na yanayotendeka katika jamii ndani ya mazingira halisi (Wamitila, 2003); Pedro (2009); Taghizadeh (2014). Mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia hii ni Georg Lukacs aliyeamini kuwepo kwa uhalisi katika ukamilifu wake. Kwa mantiki hii basi, uhalisia unamwona binadamu kama zao la ulimwengu unaomfanya aonekane katika jamii.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia ambayo huangazia maisha halisi ya jamii bila kupamba mambo. Nadharia ya Uhalisia inasaidia kuchunguza jinsi kazi hizi za fasihi zinavyoakisi ukweli halisi wa maisha ya vijana, changamoto zao, na matarajio yao bila kupamba mambo. Hii inaruhusu uchambuzi wa kina wa masuala kama vile ufisadi, ukosefu wa ajira, na migogoro ya kijamii kama inavyoonekana katika tamthilia za; *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha*. Kwa mujibu wa nadharia ya uhalisia, mwandishi anasawiri hali halisi kuhusu mazingira ya vijana katika nchi za ulimwengu wa tatu ambapo vijana hawana ajira, uongozi mbovu, ufisadi, mila na desturi na migogoro anuwai ya kifamilia. Kuhusu uhalisia wa kihisia, mwandishi anatuchorea wahusika vijana wenye hasira na huzuni lakini wenye matumaini kuhusu mabadiliko katika jamii. Kuhusu uhalisia wa kijamii, mwandishi anasawiri mazingira halisi ambamo vijana wamezaliwa, wamelelewa na ambamo wanaishi, mathalani; ukosefu wa ajira, uongozi mbovu, na migogoro ya kifamilia. Kwa upande mwingine, uhalisia wa kihisia, wahusika vijana wanadhihirisha hisia halisi kama hasira, huzuni na matumaini ya kuwepo kwa mabadiliko katika jamii. Waaidha, katika uhalisia wa kisiasa, vijana wamejitokeza kama wakosoaji wa mfumo wa utawala na wanaharakati wa mabadiliko. Kwa hivyo, nadharia ya uhalisia hujikita katika kusawiri hali halisi ya maisha ya wanajamii katika mazingira na mikitadha halisi. Fauka ya hayo, nadharia hii hulenga kufichua namna fasihi inavyoweza kuwa kioo cha jamii.

## 5.0 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulikuwa wa kiuthamano. Mbinu za ukusanyaji wa data zilikuwa ni kuhakiki matini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Tamthilia mbili; *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha* zilihakikiwa kwa kina ili kubainisha mada, wahusika vijana, maudhui yanayowahusu, mbinu za lugha na ujumbe mkuu unaohusu sauti ya vijana. Nyaraka za maktabani zilirejelewa ili kumjenga mtafiti kinadharia. Uhakiki ulizingatia:

## 6.0 Sauti ya Vijana katika Tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha*

Dhana ya "Sauti ya Vijana" inarejelea njia na mikakati mbalimbali ambayo kupitia kwayo mawazo, maoni, hisia, uzoefu, na matarajio ya watu walio katika umri wa ujana huwasilishwa, kutambuliwa, na kushirikishwa katika jamii au mifumo ya mamlaka. Sauti hii ni zaidi ya matumizi ya maneno tu; inahusu uwakilishi kamili wa kizazi hicho katika:

### 6.1 Uwakilishi wa Mawazo na Mtazamo

Hii inajumuisha mitazamo na maoni yao kuhusu masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kitamaduni. Inahusu jinsi vijana wanavyochambua na kuelezea changamoto zinazowakabili, na suluhisho wanazopendekeza. Hii ni ithibati ya

anayosema Mbuguni (1996) kuwa fasihi huwasilisha ujumbe wa msanii kwa jamii kwa lengo la kuelimisha na kuonya. Inatumika kama njia ya ufunzaji na kurekebisha tabia, huku ikiunda maadili mapya katika jamii. Tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha*, zimesawiri hili kupitia kauli, mjadala, na migogoro ya wahusika vijana katika jamii.

Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, vijana kama Neema na Asna wanawakilisha kizazi kinachotafuta maana ya maisha katika mazingira magumu. Mhusika Neema katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha* anawakilisha sauti ya vijana ambao wamekulia katika mazingira magumu, ya uchochole na ya kukatisha tamaa. Licha ya hali hii, wazazi wake walijizatiti kwa udi na uvumba kumsomesha na hatimaye akapata ajira. Neema ni kielelezo cha vijana waajibikaji, kwani anajitolea kuwasaidia wazazi wake kwa hali mbalimbali, kwa mfano, anamsomesha mdogo wake Asna hadi chuo kikuu, anagharamia matibabu ya wavyele wake na kuwaajiria wafanyakazi ili kuwasaidia katika shughuli za nyumbani. Arege (2022:2) Sara mamake Neema anasema;

> *…Lakini huyu mtoto naye, pamoja na mzigo wa familia yake anajaribu kiasi chake. Amewafaa wanuna wake kwa hali na mali.Ninasikia kulipia elimu ya chuo kikuu si lelemama. Jambo hili limewashinda hata wanaume wenye mishahara minono serekalini.*

Usemi huu ni dhihirisho kuwa, licha ya Neema kuzaliwa na kulelewa katika jamii ya mfumo-dume, msanii amemtumia mhusika huyu na uhusika wake kujenga na kuendeleza sauti ya kijana wa kike mwenye bidii masomoni na pia, mwajibikaji. Kwa mantiki hii, Neema ni kielelezo cha sauti ya vijana wa kike ambao wamekata silisila za mila na mitazamo iliyopitwa na wakati. Waaidha, Neema anawakilisha sauti ya vijana ya kupigania mabadiliko ili kujenga jamii yenye usawa wa kijinsia. Hata pale ambapo babake anasema kuwa Neema kama kifungua mimba ni ishara ya fimbo ya mzee anayerithi mtoto wa kwanza, kauli ambayo Sara, mamake Neema anaipinga, kwani yeye ni kielelezo cha wanawake wanaoshikilia kindakindaki mila na desturi zinazojenga na kushamirisha mfumo dume, katika Arege (2022:2) Sara anasema;

> *…fimbo wanarithi watoto wa kiume, si wa kike*
> *Huyu sasa ana kwake. Ndoa ina majukumu yake.*

Licha ya imani na mtazamo huu wa mamake, Neema anajitolea kwa hali na mali kuwahudumia wazazi wake kwa namna mbalimbali, kwa mfano, anagharamia matibabu ya wazazi wake, ithibati ya kijana wa kike anaewajibika kwa wazazi na jamii kwa jumla. Katika Arege (2022:2) Sara anakiri;

> *…Ugonjwa huu usingenibakisha hata nikaona leo hii.Ulikuwa umenila kiasi cha kuniacha chichi; chichi kavu. Kwenye mwako wa jua. Hadi akaja yeye na kunipeleka Kwa wataalamu…leo nisingekuwako.*

Arege katika tamthilia ya *Bembea ya maisha* anaitumia sauti ya vijana kama motifu ya safari ya kusaka maana ya maisha. Ameisawiri jamii inayoishi katika hali ngumu, hali ambayo bila shaka inawahitaji vijana kubadili mtazamo wao wa kiulimwengu ili kukabiliana nayo. Kwa mfano, ardhi wanayomiliki wanajamii si toshelevu, kwani haiwezi kukidhi mahitajji ya shughuli mbalimbali za kilimo, kwa hivyo kuna uhaba wa chakula. Kwa mfano, katika Arege (2022:5), katika mazungumzo baina ya Dina mamake Kiwa kuhusu ugumu wa maisha na matokeo yake kwa hali ya afya ya Kiwa, Dina anasema;

*…Pamoja na hali ngumu iliyopo, bado hatujafikia pa kukosa mlo wa kimsingi. Ndiyo hatumudu viliwa vya samli lakini hatuwezi kuishi kana kwamba tunazongwa na njaa. Tazamaulivyokonda. Unaelekea kushindana na ng'onda. Hiyo nafasi ya ng'onda unaitaka kwa nini?*

Kauli hii ya mama inamgusa mwanawe Kiwa, ambaye anasema sivyo anavyofikiria mamake. Kwani yeye kama kijana, licha ya ugumu wa maisha lazima abuni mbinu mbadala ya kukabiliana na hali hiyo. Kiwa anasema;

> *Dunia ya leo haithamini kimo, inathamini akili.*
> *Haitaki kututumua misuli, inataka tambo na fikra. Haya mama, mwone Neema binti Yona. Si kifyefye tu. Lakini chuma cha reli…*

Usemi huu ni ithibati ya sauti ya vijana inayodhihirisha kupevuka kwa akili, hususan kuiona dunia kwa mtazamo tofauti na wazazi wao. Mtazamo huu unaashiria sauti ya mabadiliko ya fikra katika muono ulimwengu wa vijana kuhusu ulimwengu wao. Aidha, hii ni sauti iliyojaa matumaini na mabadiliko katika jamii, sauti ambayo haioneshi sababu zozote za kukata tamaa.

Kuhusu maisha, Neema anayamithilisha na safari ya mbali, yenye misukosuko ya hapa na pale, ambayo kwa namna ya pekee kila mja huhitajika kuwa mvumilivu *(Bembea ya Maisha*, uk 29) Neema anasema:

> …*Wakati mwingine maisha hukufanya kujisikia kama abiria kwenye gari liendalo kwa kasi. Unatamani dereva apunguze mwendo lakini unakumbuka kuwa safari bado ni ndefu na hutaki kufika ukiwa umechelewa. Basi unatulia japo ndani una wasiwasi hutulii.Lakini huwezi kushuka maana safari itaganda. Kwa hivyo unajitahidi tena, japo wakati mwingine unajikuta umetambaliwa na uchovu, shaka na tuhuma…*

Katika kulinganisha maisha ya mjini na kijijini, Sara anasema afadhali ya kijijini, mtazamo ambao Asna mwanae hakubaliani nao, kwani anasema, japo wana matatizo yao mjini lakini afadhali kuliko ya kijijini ambako hamna ajira wala chochote cha kufanya. Mjadala wa Sara na mwanae Asna (Bembea, uk.31) unadhihirisha mitazamo kinzani kati ya vijana na wazee wao ambao wanasawiriwa kama wahafidhina. Waaidha, mazungumzo haya yanadhihirisha sauti ya vijana ya kudai mabadiliko ya fikra kuhusu hali anuwai za maisha. Asna katika (Bembea, 31) anasema;

> …*Kwanza mtaa huu si kila mtu anayeweza kuuishi.Chumba hiki kinaonekana kidogo lakini kodi yake ni sawa na inayolipiwa nyumba ya vyumba viwili. Katika mitaa mingine…Kijijini nitarudi na elimu yote niliyoipata? Watu watashangaa.*

Kauli hii inadhihirisha namna vijana wanavyokamia kuishi katika mitaa ya kifahari baada ya kupata elimu ya juu, hivi kwamba, wako radhi kuishi katika chumba kimoja katika mitaa ya kifahari kuliko kuishi kwenye nyumba kubwa katika mitaa ya wachochole. Kwa upande mwingine hawapo tayari kurudi kijijini baada ya kuhitimu elimu ya Chuo Kikuu. Hata hivyo, Sara anamwambia Asna kuwa “Msafiri kafiri ingawa tajiri’ falsafa ambayo Asna anaipinga kwa kusema kuwa heri kuishi masikini mjini kuliko kurudi kijijini kwenye umaskini wenyewe. Isitoshe, mazungumzo ya Sara na mwanae Asna yanadhihirisha sauti ya vijana inayoendeleza mabadiliko ya kifikra, hususan kutia bidii maishani, ili kukabili changamoto zilizowakumba wavyele wao. Kwa mfano Asna anasema;

> …*Hiyo tabu yote mliyojipa kutusomesha ina faida gani kama tutarudi huko vijijini na kuishi kama yeyote yule? Maisha ni kujaribu. Kwa kina sisi mahuluku taabu sawa na mtu aliyetapatapa kwenye mafuriko lazima kushikilia chochote na popote mradi upate kusalimika.*

Huu ni usemi unaothibitisha sauti ya vijana ambao wako tayari kukabiliana na vizingiti vyovyote katika safari ya maisha ili kufikia azma zao za maisha bila kukata tamaa. Kuhusu usasa hasa wa umbo na sura, Asna anamsikitia mwanae alivyokonda mithili ya ng’onda, kwani hatulii daima yuko mbioni kusaka natija yake haba, jambo ambalo linamfanya Asna kucheka na kusema;

> *Huelewi mama. Zilikuwa zama hizo.Yaani zilizopendwa. Sura ya leo ni hii…Wengi wanang’ang’ana kuwa hivi Lakini wameshindwa.*

Tamko hili linamchekesha sana Sara, na kusema kuwa huo ni ujinga wa watoto wa siku hizi ambao wanang’ang’ana kuwa vifyefye eti ndio urembo ilhali ni njaa tupu! Hata hivyo, Asna anamwambia kuwa hajui anavyopendeza, akitoka kibandani hakuna anaejua anaishi vipi, wanalolijua ni kwamba anatokea mtaa wa kifahari.

Kuhusu Imani, itikadi na desturi za jamii, kuna baadhi ya vijana wamezirithi na kuzishikilia kindakindaki, kwa mfano, Bunju mumewe Neema, ambaye anaona muhali kukaa nyumba moja na mamamkwe wake, kisa ni kinyume na mila na desturi za jamii yake. Hata hivyo, Neema na Asna wana mawazo ya kimabadiliko kwani wanaziona baadhi ya mila, itikadi na desturi za jamii kuwa zimepitwa na wakati. Kwa mfano; Asna (*Bembea ya Maisha, uk.35)* anasema;

> *Lakini mama nyumba yote hiyo na nafasi yote hiyo anaona muhali wewe kulaza ubavu wako humo? Wewe uliyempa binti. Tena binti mwenye kisomo si haba!*
> *Digrii mbili ni mchezo? Basi kama huo ndio umalaika, haufai pesa mbili. Ni shemeji yangu lakini ushemeji una thamani ukiwa na undugu.*
> *Neema anaonekana kukubaliana na hali hii, japo shingo upande, kwani anasema; Hata mimi hili huniuma lakini nifanye nini? Hulazimika mara kwa mara kuuwinga moyo wangu. Kila mara hujikumbusha kuwa mnyonge msonge.Ila ninashukuru aliutetea uhai wangu…*

Neema anawakilisha sauti ya vijana ambao wamo kwenye ndoa, licha ya changamoto wanazokabiliana nazo wanapiga moyo konde na kuhakikisha kuwa ndoa kama asasi muhimu katika jamii inasimama. Kwa mfano, Asna anaposema kuwa hamna haja ya mtu kuwa mtumwa katika

ndoa, Neema anasema kuwa si utumwa kwani anajitahidi kuishi kwa kutambua kuwa jana yake kama ilivyo leo ni muhimu kwa mstakabali wake. Anaendelea kusema kuwa walau ameachiwa upenyu wa kuutumia mshahara wake atakavyo, na kilicho muhimu ni kuutumia kwa ajili ya matibabu ya mama yake, haijalishi mama atalala wapi wala atakosa kulala wapi kilicho muhimu ni kuimarika kwa afya ya mama yake mengine yatapita kama upepo.

Hii ni sauti ya kujali na kuthamini afya ya wavyele licha ya vikwazo mbalimbali vinavyotokana na mila na desturi za kijamii. Fauka ya hayo, Sara anawashauri Neema na Asna wasimwone Bunju kama mume na shemeji bali wamchukulie kama ndugu yao na wote ni watoto wake, kwani Neema na Bunju tayari wamewajengea nyumba huko kijijini. Hata hivyo, Asna na Neema kwa kushadidia mtazamo na msimamo wao wa kimabadiliko wanasisitiza kuwa baadhi ya mila, itikadi na desturi za kijamii zimepitwa na wakati na kuna haja ya kuangazwa upya.

Sauti ya vijana inadhihirisha hali ngumu ya maisha hata kwa wale ambao wana kipato baada ya mwezi, hivi kwamba mshahara hautoshelezi mahitaji binafsi na wanaowategemea. Hali hii inawalazimu kuishi katika mikopo, kwa mfano Neema analazimika kumuomba mumewe amkopeshe kiasi fulani cha hela kwa ajili ya kugharamia matibabu ya mamake, kwa kuonesha namna kipato hakitoshelezi mahitaji Bunju akimjibu mkewe Neema *(Bembea ya Maisha,* uk.40) anasema:

> *Ninataka sana lakini mwenzio siwezi*
> *Afadhali wewe ambaye ndiyo hivi unaanza kukopa.Mimi nina madeni chungu nzima lakini nimeyazika moyoni.Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele. Maana huwezi kushitakia hali yako kwa kila mja. Kama kitabu huficha yaliyomo seuze binadamu?*

Baada ya usemi huu, Bunju anakumbuka kuwa alikuwa na miadi na bwana mmoja waliosoma nae katika shule ya upili ambaye ni mkurugenzi katika kampuni fulani aliyoianzisha. Walikuwa wamekubalia kuwa aende kumsaidia kwa jambo fulani, hivyo alimwahidi mkewe Neema kuwa endapo litatimia angepata hela ya kumpiga jeki kugharamia matibabu ya mamaye. Ahadi hii inahuisha amani ya moyo wa Neema na kukiri kuwa mumewe Bunju ni zawadi nzuri kwao. Aidha, aneleza namna Bunju alivyookoa maisha yake (*Bembea ya Maisha,* uk.41)

> *Hebu fikiri! Umepata ajali mbaya, inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa Imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors; ndege inafika kukupeleka*
> *Hospitali. Mwenyewe huyu analipa kila kitu, ninakwambia kila Kitu! Mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?*

Hii ni sauti ya kijana anayekumbuka na kushukuru kwa wema aliotendewa na kijana mwenzake ambaye baadaye walioana. Isitoshe, Bunju anawakilisha vijana ambao wako tayari kuwajali na kuwatendea wema binadamu wenzao. Mwandishi amewatumia wahusika hawa na uhusika wao kujenga kizazi kipya kinachojali na kuendeleza falsafa ya mtu ni utu, kwa mfano katika *Bembea ya Maisha*, uk.42 Neema anasema afadhali mifuko ifilisike lakini maradhi yasifilisi afya ya mamake, usemi ambao kwa namna ya pekee unadhihirisha kuwa afya ya mwanadamu ni muhimu zaidi kuliko pesa. Aidha, mwandishi amemtumia mhusika Neema kuendeleza itikadi za Imani ya kidini, hususan anaposema kuwa madaktari wanatoa tiba nzuri naye Mungu huponya.

Kuhusu hali ya matibabu mjini na kijijini, mwandishi amewatumia vijana Asna na Neema kudhihirisha namna utabaka ulivyoshamiri katika jamii. Sara anakiri kuwa huduma za hospitali za mjini ni nzuri hata kuliko hotelini kwani kuna; kitanda kizuri, godoro zuri, shiti safi zilizopigwa pasi na zinazobadilishwa kila mara ilihali za kule kijijini ni mithili ya seli, ukilazwa tayari wewe ni mahabusu. Asna na Neema kwa kukubaliana na mawazo ya mama yao wanatuchorea taswira halisi ya hospitali za kijijini na za mjini. Kwa mfano kuhusu kulazwa katika hospitali za kijijini (*Bembea ya Maisha,* uk. 42) Asna anasema;

> *Ukilazwa tayari huwa umeonja seli.*
> *Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari! Unashindwa kama Uuguze moyo ama ugojwa. Katika wodi hewa*
> *Iliyojaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri*
> *Mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi*
> *Matumaini ya kutoka ukiwa bora. Matumaini*
> *Yanadidimia. Tumaini lako unaliweka katika sala.*

Kwa upande wake Neema, hamna sababu ya utofauti huu, huduma ya matibabu inapaswa kuwa sawa mjini na kijijini. Hii ni sauti ya kudai

mabadiliko katika jamii kwa kushamirisha juhudi zinazojenga na kuendeleza usawa wa wanajamii bila kujali iwapo wanaishi kijijini au mjini.

Katika Jiji la Cheneo, hali ni ya kusikitisha, inawabidi madaktari na wauguzi kutumia mbinu mbadala kuwahudumia wagonjwa. Siki katika (Mstahiki, uk, 6) anamwambia Waridi amwandalie mtoto mgonjwa mchanganyiko wa sukari na chumvi katika maji moto, hata hivyo Waridi unamshangaa daktari Siki na kumuuliza hayo ni matibabu gani? Daktari Siki anasema;

> *Mwandalie tu. Dawa tulizonazo ni pain killers tu!Afadhali kufanya jambo kuliko kutofanya kabisa.Labda itawezesha mshumaa kuwaka hadi meli zinazosubiriwa zimalize kupambana na mawimbi*
>
> *…Waridi wawashie taa ya tumaini. Ganga ganga za mganga huleta tumaini.Ugumu wa hali ya maisha*

Katika *Bembea ya Maisha*, sauti ya vijana inajidhihirishwa kupitia maudhui yanayohusiana na maisha magumu na changamoto za kiuchumi ambazo vijana wanakumbana nazo. Hapa, wahusika wanatoa taswira halisi ya umaskini, ukosefu wa ajira, na matamanio yao kwa maisha bora. Vijana hawa wanatumia lugha yenye nguvu kuwasilisha hisia zao kuhusu hali yao, wakionyesha hasira na kutokuwa na matumaini kutokana na mazingira magumu wanayoishi. Tamthilia hii inatoa nafasi kwa vijana kujieleza kuhusu ndoto zao na matarajio yao katika jamii ambayo mara nyingi inawaangalia kama watu wasio na uwezo. Isitoshe, tamthilia ya *Bembea ya Maisha* inatoa mtazamo wa kina kuhusu mapambano ya wanawake vijana katika jamii yenye mifumo dume. Sauti ya vijana wa kike inawakilishwa kupitia uzoefu wa Neema, ambaye anajitahidi kuvunja minyororo ya umaskini na mila potofu. Tamthilia hii inasisitiza umuhimu wa elimu kama chombo cha ukombozi na uwezeshaji wa wanawake vijana. Kwa hivyo, kazi hizi mbili zinaonyesha kwamba sauti ya vijana ni muhimu katika kufichua matatizo mbalimbali yanayowakabili watu wa kizazi hiki. Katika *Mstahiki Meya,* Daktari Siki na Nesi Waridi wanawakilisha vijana wanaopinga uongozi mbovu uliokitwa katika ubinafsi, dhuluma na ufisadi. Wanajitokeza kama wapambanaji wa haki na maadili katika jamii.

### 6.2 Uwakilishi wa Uzoefu na Maisha Halisi

Hegel (1979) anasisitiza kazi inayosimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inavyokaribiana sana na hali iliyoko katika jamii. Uwakilishi wa uzoefu na maisha halisi inajumuisha kuonyesha hali halisi ya maisha wanayoishi vijana: kutoka kwa matatizo ya ukosefu wa ajira na elimu duni, shinikizo la wenzao na migogoro ya kizazi. Katika muktadha wa uhalisia, sauti hii hufichua ukweli mchungu wa jamii. Kuhusu maendeleo ya nchi za Kiafrika, mwandishi anamtumia mhusika Neema kutudokezea changamoto zinazokabili maendeleo katika jamii, anasema kuwa nchi nyingine zimekuwa na maendeleo ya barabara za misimu yote, ulimwengu umeendelea lakini jamii yake inaendelea kuwa tegemezi, Kuhusu baadhi ya changamoto na vizingiti vya maendeleo ya nchi za Kiafrika Neema katika (*Bembea ya Maisha*, uk.65) anasema;

> *...Ulimwengu umeendelea lakini sisi tunausindikiza tu. Tunasubiri uzalishe sisi tutumie. Wanaozalisha wanavuna*
> *Lakini sisi hapa tupo pale pale. Kwenye hujuma na kuchimbana, Kwenye ugomvi na mivutano, kwenye chuki na uhasama wa kitoto, kwenye tembo na gumzo lisiloisha, kwenye uchimvi na kusutana. Haya ndiyo maendeleo yetu.*
>
> *Tunasubiri akili kubwa kuzalisha vya kutumiwa na ulimwengu mzima na sisi biashara yetu ni maneno ya kuvuta nyuma azma ya kujiendeleza.*

Hii ni sauti ya vijana inayosuta kutowajibika na utegemezi wa jamii hususan za vijijini kwa wale walio mjini, hali ambayo bila shaka inasababisha jamii kurudi nyuma kimaendeleo. Neema anaendelea kusema kuwa watu wamechukua nafasi zao katika mtandao mzima wa nchi, zilizobaki ni chache na zinang'ang'aniwa ilhali katika mazingira ya vijijini mwanamume hasa ni yule ajuaye gongo lilipo na kujitolea kutumia hela yake yote kulinunua. Huu ni usemi ambao unadhihirisha hali halisi katika jamii, hali ambayo bila mikakati endelevu ya kuibadilisha, jamii itaendelea kurudi nyuma. Aidha, usemi huu unadhihirisha namna wanaume wengi wanashindwa kutekeleza majukumu yao ya kifamilia kwa sababu ya utumwa wa pombe. Sauti hii ni ya kimabadiliko hasa kila mwanajamii kuwajibika katika shughuli anuwai za kimaendeleo katika jamii bila kujali tofauti za kijinsia ambazo zinashamirishwa na kuendelezwa na mifumo, mila desturi na tamaduni za kijamii.

Kwa upande wa *Bembea ya Maisha*, matokeo yanaonyesha changamoto za kijamii na kiuchumi zinazowakabili vijana, hasa wanawake vijana, katika kutafuta nafasi yao katika jamii. Wahusika kama vile Neema wanakabiliana na shinikizo la kijamii, umaskini, na matatizo ya kifamilia, huku wakijitahidi kujenga maisha yao. Tamthilia hii inaangazia umuhimu wa elimu na kujitegemea kwa vijana wa kike.

### 6.3 Jukumu la Ushiriki na Ushawishi

Sauti ya Vijana inasisitiza kwamba vijana hawapaswi kuwa waathirika tu au wapokeaji wa maamuzi, bali wanapaswa kuwa washiriki hai na wenye uwezo wa kushawishi maamuzi yanayowaathiri wao na jamii kwa ujumla. Tamthilia huonyesha hili kwa kuwapa vijana jukumu la kupinga udhalimu au kuchochea mabadiliko. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, vijana Siki, Waridi na Tatu wamesawiriwa kama vijana wapambanaji hususan dhidi ya uongozi mbovu ulioshamiri ubinafsi na ufisadi. Uhusika wao umelenga katika ujenzi wa jamii yenye usawa, haki na maadili.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mwandishi anawatumia wahusika Siki na Waridi kuchora taswira ya jinsi hali ilivyo katika jiji la Cheneo, madawa ni haba, na wala hamna taarifa za kuaminika kuhusu lini madawa yaliyoagizwa yatafika hosipitalini. Sauti ya vijana hawa inatuchorea hali ya utegemezi uliokithiri wa nchi za Kiafrika kwa mataifa ya Ulaya, suala ambalo linachangiwa na ufisadi na uongozi mbovu. Kutokana na ukosefu wa dawa za kutosha inawalazimu madaktari na wauguzi kuwahudumia baadhi tu ya wagonjwa. Kwa mfano katika (Mstahiki, uk. 2) daktari Siki anasema;

> *Haya vizuri! Naona tuwashughulikie wale ambao dawa za kuwafaa zipo…Basi mwite mgonjwa wa kwanza.*

Hata pale ambapo daktari anasema yuko tayari kuwatibu baadhi ya wagonjwa, Waridi anasema hata hao wagojwa hawana hela za kulipia huduma wanazotaka, wengine hawana hata karatasi ya kunakilia udodosi wao! Sauti hii inadhihirisha hali halisi ya umasikini wanaokumbana nao wanajamii, lakini baadhi ya viongozi wao wanajali tu maslahi yao binafsi kwa kuzidi kuwanyonya wananchi. Waridi katika *(Mstahiki Meya*. uk. 3) anasema:

> *Ni amri daktari. Kama wakubwa wenyewe wameisha. Kusema sisi tufanye nini? Si basi tu!*
> *Bora kutazama. Nchi yenyewe change kwa kila hali. Nao hao Wazungu wanahimiza mfumo wa kugawana*
> *Gharama kutumika. Sisi tutafanya nini na nchi*
> *Yenyewe maskini: ombaomba?*

Hii ni sauti inayodhihirisha ukoloni mamboleo, hata pale nchi za Afrika zinadai kuwa na uhuru, haziwezi kujikimu na kujitegemea, hulazimika kufuata maelekezo ya wazungu katika kutekeleza masuala muhimu kwa wananchi wao. Uhuru unakuwa ni wa bendera tu! Hata hivyo, mwandishi anawatumia wahusika Siki na Waridi kuthibitisha ukweli kwamba umasikini wa nchi za kiafrika ni kasumba ambayo inajengwa na kushamirishwa na wachache walio katika ngazi za uongozi.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mwandishi amemtumia mhusika Siki ambaye ni kijana katika kutetea usawa na mabadiliko ya kweli katika jamii, licha ya Siki kuwa ndugu yake Meya, hachelei kumwambia bayana hali halisi katika jamii. Anasisitiza kuwa hasemi kwa ajili ya siasa bali anamwambia ukweli kwamba wanajamii wana njaa na ni hatari kuwaongoza watu wenye njaa na kiu ya mabadiliko. Waaidha, Siki anaendeleza sauti ya vijana ya kudai uhuru wa kweli katika enzi ya ukoloni mamboleo, wa kuendesha mambo yao bila kukubali kufuata waliyoyaamua wakoloni kwa mfano, malengo ya kimaendeleo ya milenia bila kuwaridhisha wananchi. Siki katika (*Mstahiki Meya*, uk. 11) anamwambia Meya:

> *…Hizi si habari za kugoma na kutogoma. La hasha! Ni habari za hali ya maisha ya watu waliokuchaguaWewe kwa kuamini kuwa utaziboresha hali zao. Watu wanakulilia. Wanataka uwasikilize.*
> *Hali yao ya maisha ni ngumu. Wanashindwa kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe hakuna. Gharama za*
> *maisha zinazidi kupanda na mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali mishahara haipandi…*

Hata hivyo, Meya anaonekana kutojali na anayomwambia daktari siki na badala yake anasema kwa kiburi kuwa baraza analoliongoza lina uthabiti kuliko mabaraza mengine yaliyojirani. Hata hivyo, daktari Siki anamwambia Mstahiki Meya kuwa si vema kuilinganisha na majirani dhaifu kwani wana uwezo wa kufanya bora zaidi ya ubora wa majirani wao. Sauti ya Siki ni ithibati ya

haja ya mabadiliko ya fikra na namna ya kuwajibika katika kufikia upeo wa maendeleo kuliko kuendelea kujilinganisha na jamii nyingine, kwani kuna uhitaji wa kupiga hatua kila uchao. Mwandishi anamtumia mhusika daktari siki ambaye ni kijana katika kuchora hali halisi ya umasikini unaotokana sera mbovu zinazojengwa na kuendelezwa na viongozi ambao hawajali hali za wananchi wao. Siki anasema watu wana shida, wengi wanakufa kwa njaa kwa sababu hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi, hivi kwamba hata sembe na sukuma vinawatoa jasho kuvitia mezani. Isitoshe daktari Siki anamwambia Mstahiki Meya;

***Siki**: Kweli ni jana tu kitoto kidogo kimenifia mkononi mwangu kwa njaa na ugonjwa…*

Naye, Meya kwa kiburi na kutojali na kuthamini maisha ya wanaichi wake anasema

> ***Meya**: Huyo mmoja tu! Unadhani wangapi wananiunga mkono, Cheneo ina watu wangapi?*

Katika tamthilia ya *"Mstahiki Meya,"* mwandishi Timothy M. Arege anatumia wahusika Daktari Siki na Nesi Waridi kuwakilisha sauti ya vijana katika muktadha wa matatizo ya kijamii. Daktari Siki, ambaye ni kijana mwenye ujuzi wa kitaaluma, anajitahidi kuleta mabadiliko katika huduma za afya lakini anakutana na upinzani kutoka kwa viongozi wa kisiasa ambao hawajali maslahi ya wananchi. Hali hii inaonyesha jinsi vijana wanavyopambana na mfumo dume wa uongozi ambao unawanyima fursa za kuleta mabadiliko chanya. Naye Nesi Waridi pia, anawakilisha sauti ya vijana kwa kuwa na mtazamo wa kukosoa mfumo wa ugawaji wa rasilimali za afya. Anapojaribu kuelezea hali halisi ya ukosefu wa dawa na rasilimali, anaonyesha ujasiri wa vijana kukabiliana na ukweli mgumu bila woga. Hii inadhihirisha kwamba vijana wanaweza kuwa wasemaji wenye nguvu katika jamii zao, wakikabili changamoto zinazowakabili.

Fauka ya hayo, uchambuzi wa *Mstahiki Meya* unaonyesha kuwa tamthilia hii inatoa taswira halisi ya ufisadi na siasa chafu zinazowaathiri vijana moja kwa moja. Wahusika vijana kama vile Siki, Waridi na Tatu wanajikuta katika mazingira magumu ambapo ndoto zao za maisha bora zinakandamizwa na mfumo mbovu wa utawala na siasa. Sauti yao inawakilishwa kupitia matumaini yao yaliyovunjika na juhudi zao za kupambana na dhuluma. Kwa upande wa *Bembea ya Maisha,* matokeo yanaonyesha tamthilia hii inachunguza changamoto za kijamii na kiuchumi zinazowakabili vijana, hasa wanawake vijana, katika kutafuta nafasi yao katika jamii. Wahusika kama vile Neema na Asna wanakabiliana na shinikizo la kijamii, umaskini, na matatizo ya kifamilia, huku wakijitahidi kujenga maisha yao, tamthilia hii kwa namna ya pekee inaangazia umuhimu wa elimu na kujitegemea kwa vijana wa kike.

Sauti ya vijana katika tamthilia hizi inaoana na mapendekezo ya shirika la mashinani *Shining Hope for Communities* (SHOFCO, 2025) nchini Kenya linalopendekeza kuwa sauti ya vijana inastahili kusikizwa. Isitoshe, Umoja wa Mataifa (2019) ilizindua ripoti yake ya kimataifa kuhusu vijana ikisema kuwa ushirikishwaji wa vijana bilioni 1.2 wenye umri kati ya miaka 15 – 24 ni muhimu katika kufanikisha jamii endelevu, jumuishi na thabiti.

### 6.4 Lugha na Mtindo wa Kuwasilisha

Hii inahusu njia ya kipekee wanayotumia vijana kuwasilisha ujumbe wao. Inaweza kujumuisha matumizi ya misemo ya mtaani, tamathali za usemi, migogoro ya kihisia au mitindo maalum ya mawasiliano ambayo hutofautisha kizazi chao na vizazi vingine. Katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*, mwandishi anamtumia mhusika Asna kama kielelezo cha kudai usawa baina ya wasichana na wavulana katika jamii mpya. Asna anamwambia mamake kuwa yeye ni *Tomboy*, mama anapomuuliza maana ya neno *"tomboy"*, Asna anacheka na kusema:

*Msichana anayeishi na kutenda mambo kama mvulana*.

Matumizi ya msimu *tomboy* katika kauli hii yanadokeza mazungumzo halisi yanaongeza uhalisia wa sauti za vijana. Kwa upande mwingine, Huu ni usemi unaodhihirisha namna vijana wanatumia uhuru na elimu yao katika kuendeleza mabadiliko katika jamii hususan kuhusu mila na desturi zinazojenga na kushamirisha ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii anuwai. Hata hivyo, baadhi ya vijana walio na fikra sawia na Asna wanaiona ndoa kama silisila ya utumwa iliyojaa madhila si haba, hususan kwa mwanamke. Asna anakiri kuwa anaziogopa ndoa, kwa mfano katika (*Bembea ya Maisha*, uk. 53) Asna anasema;

> *Angalia mama. Madaktari wamesema chanzo*
> *cha maradhi yako hayo. Ndoa imeyatia doa maisha yako.*

> *Imekuletea msongo wa mawazo kwa kukaripiwa na hata kupigwa na baba. Sasa mimi ninataka uhuru wangu na sitataka kupigwa kichapo cha mbwa mara kwa mara mpaka nipate ugonjwa wa moyo. Matokeo yake ni haya. Kuna raha gani kama maisha ni kugeuzwa ngoma ukapigwa kwa fujo yote mpaka ukapasuka?*

Usemi huu unadhihirisha sauti ya vijana kuhusu asasi ya ndoa, sauti inayosawiri madhila anayokabiliana nayo mwanamke katika jamii ya mfumo-dume. Isitoshe, kuhusu ndoa Asna katika (Bembea, uk. 53) anasema;

> *Mama, ajabu ya ndoa ni kwamba unafuzu na kukabidhiwa Cheti kabla ya kuukalia mtihani wenyewe. Mtihani huja baadaye. Kisha mitihani hiyo haina silabasi mahususi*

Kauli hii ni nzito inayojenga hofu ya vijana kuhusu asasi ya ndoa. Asna ni kijana ambaye ameshuhudia hali ya ndoa ya wazazi wake na dada yake Neema ambaye alipita vizuri tena kwa alama za kumezea mate lakini anapitia mitihani inayomyumbisha katika maisha yake, mitihani ambayo imedhoofisha ukakamavu na kujiamini kwa dhati. Hata hivyo, mwandishi anasema ndoa ni mithili ya bembea, kuna wakati inakuwa juu na wakati mwingine chini na ndiyo falsafa ya namna maisha yalivyo.

Katika *Mstahiki Meya,* sauti ya vijana inajitokeza kama sauti ya kukata tamaa lakini pia ya matumaini ya mabadiliko. Vijana wanawakilishwa kama kundi lililokandamizwa na mfumo wa utawala na siasa, lakini pia kama nguvu inayoweza kuleta mabadiliko. Matumizi ya lugha rahisi na yenye hisia kali inasaidia kuwasilisha hisia zao za kukata tamaa na hasira. Kauli zao zinashadidia haki na usawa katika jamii. Kwa upande mwingine, Tamthilia hizi zinatoa wito kwa vijana kujitokeza na kupigania haki zao.

Barani Afrika, sauti ya vijana imeweza kusikika mfano, nchini Kenya vijana *Gen Z* wamekuwa sauti ya mageuzi wakilenga uwajibikaji wa viongozi, uchumi bora, na kuondoa siasa za kikabila. Kundi hili lilitumia mbinu tofauti na ilivyozoeleka kama vile maandamano ya mitandaoni. *Gen Z* walitumia mitandao ya kijamii mfano, *twittet(X), tiktok* na *Instagram* kuandaa maandamano na kupasha ujumbe wa kisiasa. Vijana hawa vilevile walitumia *hashtags* kama vile *#Occupy Parliament#, #Reject Finance Bill#* na *#Gen Z Revolution#* kuhamazisha wenzao. Mbinu hizi zilidhihirisha uwezo walionao vijana na umuhimu wa kusikiza sauti zao.

## 7.0 Hitimisho

Tamthilia zote mbili zinathibitisha kuwa Fasihi ya Kiswahili ina jukumu muhimu katika kuwakilisha sauti ya vijana na changamoto zao. Tamthilia ya *Mstahiki Meya* inaangazia masuala ya kisiasa na ufisadi katika jamii, huku *Bembea ya Maisha* ikijikita katika masuala ya kijamii na kiuchumi, hasa kwa wanawake vijana. Mwandishi Timothy Arege ametumia mbinu za kifasihi kwa ufanisi kuwasilisha hisia, matarajio, na mapambano ya vijana. Isitoshe, tamthilia hizi zinatoa mfano mzuri wa jinsi sauti ya vijana inaweza kutumika kuwakilisha changamoto za kijamii katika Fasihi ya Kiswahili. Wahusika vijana katika tamthilia hizi wanaonyesha ujasiri wao katika kukabiliana na matatizo yanayowakabili wakati wakijaribu kubadilisha hali zao za maisha.

Makala hii imethibitisha kuwa *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha* ni mifano ya kipekee ya jinsi Fasihi ya Kiswahili inavyoweza kutumika kama jukwaa la kuwasilisha sauti ya vijana. Kazi hizi zinatoa taswira halisi ya maisha ya vijana, changamoto wanazokabiliana nazo, na matumaini yao ya maisha bora. Kwa kuwakilisha sauti hizi, waandishi wanachangia katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya vijana na kuhamasisha mabadiliko. Waaidha, makala hii imethibitisha kuwa Fasihi ya Kiswahili ni jukwaa lenye nguvu la kuwasilisha sauti ya vijana. Kupitia wahusika wao, vijana hujitokeza kama wakosoaji, waathirika, na wapambanaji wa hali halisi ya jamii. Fasihi hii si tu burudani, bali ni chombo cha mabadiliko ya kijamii. Kwa upande mwingine, Sauti ya vijana katika Fasihi ya Kiswahili ni muhimu kwa maendeleo ya jamii. Kupitia tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Bembea ya Maisha*, tunaona vijana wakijitokeza kama wahusika wenye msimamo, fikra pevu, na ari ya mabadiliko. Fasihi hii ni kioo cha jamii na chombo cha kuendeleza kizazi kijacho.

## *MAREJELEO*

Arege, T. (2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi. Vide-Muwa Publishers.

Arege, T. (2022). *Bembea ya Maisha*. Nairobi. Access Publishers.

Balisidya, N. M. (1987). Ufundishaji wa fasihi simulizi katika sekondari. *Mulika*, (19), 11–18.

Eagleton, T. (2008). *Literary theory: An introduction* (3rd ed.). Blackwell Publishing.

Hegel, G.W.F.(1979). *Hegels System of Ethical Life and Philosophy of Spirit*. Albany. State University of New York (SUNY)Press

Lukács, G. (1971). *History and class consciousness: Studies in Marxist dialectics*. The MIT Press.

Pedro, M. G. (2009). A Brief Intellectual History of Early Realism in *IR*: A Critical Realism. Paper presented at the International Association of Critical Realism (IACR), Rio de Janeiro, July 2009.
Mbuguni, P. (1996). *The Gender Dimension of Urban Poverty: The Case of Tanzania*. Dar es Salaam University Press.

Mohamed, S.A. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. East African Educational Publishers.

Mwangi, M. (2021). Uhalisia katika tamthilia ya Kiswahili: Uchambuzi wa Mstahiki Meya. *Jarida la Fasihi na Lugha*, 8(2), 45–59.

Ngũgĩ, T. (1986). Decolonising the mind: The politics of language in African literature.London, England: James Currey.

Njoroge, P. (2023). Sauti ya vijana katika fasihi ya Kiswahili: Muktadha wa kijamii na kisiasa. *Kiswahili Journal of African Languages and Literature*, 15(1), 78–92.

SHOFCO. (2025) Community Power Through Collective Action. *https://www.shofco.org*

Taghizadeh, Ali. (2014). A Theory of Literary Realism. Theory and Practice in *Language Studies 4, 8: 1628-1635.*

Umoja wa Mataifa *(22-02-2019).*

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Publishers.